



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

8 JULAI, 2010



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 8 JULAI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO PAMOJA NA WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Kazi,

Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

WASEMAJI WAKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO PAMOJA NA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:

Taarifa ya Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Kazi, ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**186. MHESHIMIWA NURU AWADHI BAFADHIL
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Kazi ya Askari wa Usalama katika kipindi
cha Uchaguzi ni kusimamia upigaji kura
na sehemu ya kupigia kura wala
hawapaswi kujihusisha na kuhesabu
kura:-

Je, Serikali inasema nini juu ya Askari
ambao huhesabu kura kwenye chaguzi
mbalimbali.

**187. MHESHIMIWA EPHRAIM NEHEMIA
MADEJE (DODOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Ingawa Serikali bado inayo dhamira ya
kuufanya Mji wa Dodoma uwe Makao

Makuu ya Serikali lakini bado inaendelea kuimarisha miundombinu na kujenga majengo mbalimbali Mkoani Dar es Salaam:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba, kwa kufanya hivyo haitimizi dhamira yake hali inayoweza kuwafanya wananchi wakose imani na Serikali yao;
- (b) Kama dhamira ipo; Je, Serikali inashindwaje kuweka bayana mikakati thabiti ya kujenga miundombinu muhimu kwa ajili ya kuhamisha Makao Makuu kuja Dodoma.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:

188. MHESHIMIWA MGENI JADI KADIKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:- Vyombo vya habari ni muhimu sana katika kuwaelimisha wananchi na kutoa habari mbalimbali lakini Radio ya TBC Taifa ambayo ni namba moja kwa ubora wa kutoa habari inasikika Mikoa kumi na mbili

(12) tu nchini na Mikoa mingine inakosa matangazo hayo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa, chombo hicho kinasikika nchi nzima.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

189. MHESHIMIWA JAMES DAUDI LEMBELI (KAHAMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Mji wa Kahama unakuwa kwa kasi kiuchumi lakini upanuzi wa huduma ya umeme hauendi sanjari na kasi hiyo hivyo kusababisha usumbufu mkubwa:-

- (a) Je, ni sababu gani za msingi kwa Shirika la **TANESCO** Kahama kuwafanya wananchi kusubiri kwa muda wa kati ya mwaka mmoja hadi minne kuunganishiwa huduma hiyo;

- (b) Je, ni lini maeneo ya Kata ya Kahama Mjini, Nyihogo na Kata ya Mhunga yatakata umeme kwa utaratibu wa kawaida;
- (c) Je, ni lini Serikali itaunganisha umeme wa Buzwagi na Mji wa Kahama ili kuondokana na tatizo la umeme unaotoka Ibadakuli kwenda Kahama ambao hukatika mara kwa mara.

**190. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN
MANYANYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Uwezo wa *mashine* za kuzalisha umeme wa Mbinga ni mkubwa ikilinganishwa na matumizi halisi ya sasa hasa kutokana na kukosekana/ upungufu wa mtandao wa usambazaji wa umeme (Low Voltage Distribution Network 0.4 kv na High Voltage 11 kv).

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mtandao huo kwa mwaka 2009/2010.

III. KAULI ZA MAWAZIRI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA
MICHEZO NA WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA
MAENDELEO YA VIJANA:**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**DODOMA
8 JULAI, 2010**

**DKT. T.D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**